

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULIZA LEO

MKUTANO WA PILI

KIKAO CHA NNE

29 JANUARI, 2016



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA PILI

KIKAO CHA NNE – TAREHE 29 JANUARI, 2016

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa Mwaka ulioshia tarehe 30 Juni, 2015 (*The Annual Report of Energy and Water Regulatory Authority (EWURA) for the Year ended 30th June, 2015*).

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa Kipindi cha miaka mitano kinachoanzia 2016/2017 – 2020/2021 (*The Framework of the second five year Development Plan, 2016/2017 – 2020/2021*).

MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16); pamoja na Mapendekezo ya Muundo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21).

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Mipango juu ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa Kipindi cha Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21.

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

38. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kata ya Katumba inakabiliwa na tatizo kubwa la maji linalosababisha akina mama wengi kwenda umbali mrefu kutafuta maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufikisha maji katika Kata hiyo.

39. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mkoa wa Katavi ni mmoja kati ya Mikoa iliyoanzishwa hivi karibuni ili kusogeza karibu na Wananchi huduma muhimu za Serikali lakini Mkoa huo hauna Hospitali ya Mkoa na Serikali ilishaamua kujenga hospital hiyo na serikali ya Mkoa ilishatenga eneo kwa ajili ya ujenzi:-

(a) Je, ni lini utekelezaji wa mradi huo utaanza;

(b) Jiografia ya Mkoa wa Katavi ni pembezoni mwa nchi; Je, hiyo inaweza kuwa sababu ya kusuasua kwa mradi huo na kupita takribani miaka minne sasa toka Serikali ifanye uamuzi huo lakini hakuna hata dalili chanya kuelekea kukamilika kwa mradi huo.

40. MHESHIMIWA MUNDE TAMBWE ABDALLAH (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora inakabiliwa na kero mbalimbali kama vile ukosefu wa madaktari Bingwa wa watoto, akinamama, mifupa nk; ukosefu wa vifaa muhimu kama vile ECG Mashine, CT-Scan, MRA Mashine, ukosefu wa huduma za ICU pamoja na kwamba lipo jengo zuri lakini halina vifaa vya huduma za dharura:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kutatua kero hizo zinazoikabili Hospitali hiyo kwa muda mrefu.

**41. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Sera mpya ya elimu ya mwaka 2014 inatambua upatikanaji wa elimu ya msingi bure; lakini Serikali imeshindwa kupeleka ruzuku ya shilingi 10,000/= kwa kila mwanafunzi wa shule za msingi za umma na shilingi 25,000/= kwa kila mwanafunzi wa shule za sekondari za umma:-

Je, Serikali inaweza kuweka mchanganuo wa jinsi gani itakavyoweza kutekeleza sera, hiyo mpya ya elimu ya 2014 kwa kutoa elimu bure bila kuathiri ubora wa elimu.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**42. MHESHIMIWA KASUKU SAMSONI BILAGO
(BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Kifungu cha 3 cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, na Kifungu cha 1(26) cha Kanuni za Kudumu za mwaka 2009 vinatoa tafsiri ya neno mwajiri kuwa ni mtu au taasisi ambayo mtumishi wa Umma anaingia naye mkataba wa ajira na kumlipa mshahara:-

Je, kwa kuzingatia tafsiri hiyo, Mwalimu ambaye ni mtumishi wa Umma Mwajiri wake ni nani.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

**43. MHESHIMIWA DESDERIUS JOHN MIPATA
(NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Wakati akiwa Makao Makuu ya Jimbo la Nkasi Kusini, Makamu wa Rais wa Awamu ya Tano aliwaahidi Wananchi wa Jimbo hilo mawasiliano ya simu za Mkononi kwa Kata nne za Mwambao wa Ziwa Tanganyika ambazo ni Ninde, Wampembe, Kizumbi na Kala:-

Je, ni lini utekelezaji wa ahadi hiyo utafanyika.

**44. MHESHIMIWA MAULID SAID ABDALLAH
MTULIA (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kufuatia upanuzi wa barabara ya Kilwa mwaka 2002, wapo Wananchi 80 waliolipwa maeneo ya Kongowe mwaka 2008 na wengine 111 walilipwa baada ya hukumu ya shauri lililofunguliwa na Ndg. Mtumwa:-

Je, Serikali itakamilisha lini malipo ya fidia ya nyumba zote zilizobomolewa kupisha upanuzi wa barabara hiyo.

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

45. MHESHIWA KANGI ALPHAXARD LUGOLA (MWIBARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Mapambano dhidi ya uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi yamekuwa yakihusisha pia njia ya kuwanyang'anya zana haramu wavuvi wadogo kupitia mradi wa MANCEP na kuwapatia zana za uvuvi zinazoruhusiwa:-

- (a) Je, mradi huo umefanikiwa kwa kiwango gani;
- (b) Kama umefanikiwa; Je, ni lini mradi huo
 - utanzishwa kwa wavuvi wadogo wa Jimbo la Mwibara katika Ziwa Victoria.

46. MHESHIWA HAMIDU HASSAN BOBALI (MCHINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Wakulima wengi Mkoani Lindi wameamua kujikita katika zao la Ufuta ambalo ndilo zao la biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima hao kupata pembejeo kupitia mfuko wa Taifa wa Pembejeo.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

47. MHESHIMIWA SUSAN ANSELM LYIMO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:- Mwishoni mwa Mwaka 2015 Haki Elimu walitoa tathmini ya utafiti wa Elimu kwa kipindi cha miaka 10 ya Awamu ya Nne na kugundua ongezeko kubwa la udahili kwa ngazi zote na kuporomoka kwa ubora wa Elimu:-

- (a) Je, ni kwa kiasi gani utafiti huo umeakisi uhalisia wa hali ya Elimu hususan ile ya Sekondari;
- (b) Je, Serikali ya Awamu ya tano ina mikakati gani ya kuinua ubora wa Elimu hapa nchini.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:

48. MHESHIMIWA ALI HASSAN KING (JANG'OMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani:- Serikali ina mpango wa kutatua tatizo la makazi kwa Askari wa Jeshi la Polisi na Mheshimiwa Rais aligusia azma hiyo alipokuwa akilihutubia Bunge hili la Kumi na Moja kwenye kikao cha ufunguzi :-

Je, Serikali imepanga kujenga Mikoa mingapi majengo hayo ikiwemo Zanzibar.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

49. MHESHIMIWA HAMIDA MOHAMED ABDALLAH (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Vijana wengi wa Mkoa wa Lindi karibu 40% hawana ajira kutokana na ukosefu wa viwanda mkoani humo; na kwa kutambua kuwa sehemu kubwa ya uchumi wetu unategemea kilimo na Serikali ilitunga sera ya maendeleo endelevu ya viwanda ya mwaka 1996 – 2020 itakayosimamia maendeleo ya viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ili kuongeza thamani ya mazao:-

Je, sera hiyo imesimamiwa vipi katika kuvifanya viwanda vilivyopo vya usindikaji wa mazao viendelezwe ili kuongeza thamani ya mazao yetu na kukuza uchumi na hatimae vijana kupata ajira katika Mkoa wa Lindi.

50. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:-

Je, ni lini Serikali itasimamia kwa dhati sheria zake na kuondosha unyonyaji na ukandamizaji unaofanywa na wachuuzi kwa kununua mazao ya Wakulima kwa utaratibu wa kufunga rumbesa.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

51. MHESHIMIWA FATUMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):

Atamuuliza Waziri wa Katiba na Sheria:- Baadhi ya Sheria nchini ikiwemo sheria ya mirathi ya kimila, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 pamoja na sheria ya hali za watu zimekuwa na upungufu mkubwa hivyo kuhitaji kutazamwa upya ili kufanyiwa marekebisho:-

Je, Serikali ina nia gani ya dhati ya kuwasaidia wanawake na watoto wa kike kwa kuzifanyia marekebisho sheria hizo kandamizi na za kibaguzi hasa ikizingatiwa kuwa nchi yetu imeridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa na ya kikanda juu ya masuala ya kuondoa ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto.

52. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Hivi karibuni Jimbo la Kigamboni limetangazwa kuwa Wilaya mpya, hata hivyo Wananchi wake bado wanapata huduma ya Mahakama kupitia Wilaya ya Temeke:-

- (a) Je, Serikali itaanzisha lini Mahakama ya Wilaya ya Kigamboni;
- (b) Je, utekelezaji wa hatua hiyo utanza lini.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba Bunge sasa lijadili na kuidhinisha Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa kwa Kipindi cha miaka mitano kinachoanzia 2016/2017 – 2020/2021 (*The Framework of the second five year Development Plan, 2016/2017 – 2020/2021*).

DODOMA
29 JANUARI, 2015

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE